

Mimea Vamizi Afrika Mashariki

Kutathmini na kukabiliana na athari zake kwenye mazingira na maisha

<http://www.woodyweeds.org/>

Madhara ya Mvuti (Lantana) kwenye maisha ya watu eneo la Amani na usimamizi endelevu wa ardhi ili kukabiliana na athari zake



Mvuti uliletwa Afrika Mashariki miaka mingi iliyopita kama mmea wa bustanini na umepandwa kwa wingi sehemu mbali mbali kuzunguka maeneo ya makazi. Mvuti unatumika kama fensi ya nyumba, kuni na malisho ya wanyama. Pia inasemekana Mvuti hurutubisha ardhi.



"Kwenye eneo la Mashariki ya Usambara nilitumia picha za satelaiti kuangalia ukubwa wa eneo lililovamiwa na Mvuti na pia jinsi unavyoweza kuathiri mazao."

Amina Hamadi, mwanafunzi wa shahada ya uzamifu katika chuo cha kilimo Sokoine (Morogoro)

Katika eneo la Amani, mvuti umeenea katika mashamba, ambapo inashindana na mazao. Uwepo wake unaongeza gharama za utunzaji, kwakua kuiondoa Mvuti kunahitaji nguvu kazi kubwa au dawa za magugu. Sehemu mivuti ilipovamia, mimea ya asili imepungua na bioanuai kwa ujumla.




Tumeonyesha hali ya sasa ya usambaaji wa Mivuti Afrika Mashariki na maeneo ambayo yako katika hatari ya kuvamiwa na Mivuti. Tunachunguza athari za huu mmea katika mazingira, watu na uchumi. Tunatathmini ni jinsi gani athari hizi zinabadilika endapo eneo lililovamiwa na mivuti litaongezeka.

Katika eneo la Amani, tunatathmini athari za mivuti katika ukuaji wa mazao na mimea mingine, athari katika uwepo wa wadudu na katika hali ya udongo. Pia tunatathmini ni kwa jinsi gani mivuti inaathiri vipato vya watu na kubadilisha kiasi cha mavuno na gharama za uzalishaji.



Mradi wetu utasaidia jamii sehemu mahalia, mashirika yasiyo ya kiserikali na mamlaka husika kuchagua mpango mzuri wa kupunguza athari hasi na kuongeza faida za mivuti. Kwa madhumuni haya, tutatambua na kuhamasisha matumizi endelevu ya ardhi katika eneo la Amani.

More information: Dr John Richard, TAFORI: +255 715 811 618 or Prof George Kajembe, Sokoine University of Agriculture: +255 654 165 656



Swiss Programme for Research
on Global Issues for Development



Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra
Swiss Agency for Development
and Cooperation SDC



SWISS NATIONAL SCIENCE FOUNDATION